

## **HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

### **Kusimamia uingizaji wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo.**

Idara inatoa vibali vya kusafirisha mifugo ndani ya nchi ambapo usafirishaji utanyika ndani na nje ya Wilaya na Mkoa na vivyo hivyo na kwa mazao yatokanayo na mifugo.

- Msafirishaji anatakiwa kulipia gharama za usafirishaji katika akaunti ya Manispaa kulingana na idadi ya mifugo anayotaka kuisafirisha kwa wakati husika ndipo apewe kibali. Viwango vya gharama vinatofautiana kulingana na aina ya mifugo na kama anasafirisha nje ya Mkoa. Vibali vya kusafirisha kuku hutolewa bure.
- Katika kufanya utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo na kuyabaini na kupanga mkakati wa kuyatokomeza kama vile

kufuatilia kwa karibu ripoti za watu waliong'atwa na mbwa kwa kuwapa vibali kwa ajili ya kwenda kutibiwa hospitali na kumbukumbu zao huwekwa kwenye faili hapa ofisini ikiwa pia kuchukua hatua pale inapobidi kwa mbwa kutegemeana na chanzo cha kusababisha tatizo.